



REPUBLIC OF KENYA

Taarifa ya Maongozi Rasmi ya Serikali Nambari 3 ya Mwaka 2012

TOLEO MAARUFU



SERA YA IDADI YA WATU KWA USTAWI WA TAIFA

MINISTRY OF STATE FOR PLANNING,
NATIONAL DEVELOPMENT AND VISION 2030

**Taarifa ya Maongozi Rasmi ya Serikali
Nambari 3 ya Mwaka 2012**

TOLEO MAARUFU

**Sera ya Idadi ya Watu Kwa Ustawi
wa Taifa**

Utangulizi	iii
1.0 Nguzo za Sera ya Idadi ya watu kwa Ustawi wa Taifa	1
2.0 Idadi ya Watu na Hali ya Kijamii na Kiuchumi	2
3.0 Matokeo ya Sera za Idadi ya Watu ya Awali	3
3.1 Juhudi za Awali	3
3.2 Mambo yaliyochangia ufanisi na pingamizi za utekelezaji sera za awali	4
3.3 Changamoto zilizopo na zinazochipuka kwa mipango inayoshughulikia idadi ya watu	5
4.0 Maswala kuhusu idadi ya watu na mapendekezo ya hatua za kuchukuliwa	6
4.1 Mfumo wa Idadi ya watu Nchini Kenya	6
4.1.1 Ukubwa wa Idadi ya Watu na Ukuaji	6
4.1.2 Mpangilio wa Idadi ya Watu	6
4.2 Maswala kuhusu Mipango ya Idadi ya Watu	11
4.2.1 Habari, Elimu, Mawasiliano na Upigianjanji	11
4.2.2 Utaoji wa Huduma za Mpango wa Uzazi	12

4.3	Sehemu za Ujumbe Mkuu	13
4.3.1	Idadi ya watu na ukuaji wa uchumi	13
4.3.2	Idadi ya watu na Kupunguza Umaskini	13
4.3.3	Idadi ya Watu na Ustawi wa Mazingira	14
4.3.4	Idadi ya Watu, Teknolojia, Utafiti na Maendeleo	15
4.3.5	Idadi ya watu na Elimu	16
4.3.6	Usawa wa Kijinsia na Kuwapa Wanawake Mamlaka	17
4.3.7	Magonjwa na Vifo	18
4.3.8	Afya ya Uzazi na Haki za Uzazi	20
5.0	Lengo, Madhumuni na Shabaha ya Sera ya Idadi ya watu	21
5.1	Lengo la Sera	21
5.2	Madhumuni ya Sera	21
5.3	Shabaha za mwaka 2030	22
6.0	Utekelezaji, Uangalizi na Tathmini	24

Utangulizi

Serikali ya Kenya tangu ipate Uhuru imetambua kwamba usimamizi wa idadi ya watu ni muhimu katika kuafikia ustawi wa kiuchumi na kijamii. Kwa muda, serikali imebuni sera kadhaa za idadi ya watu, mikakati na mipango ya kushughulikia changamoto za usimamizi wa idadi ya watu. Sera hii ya Idadi ya watu kwa Ustawi wa taifa inafuatia Taarifa ya Maongozi rasmi ya Serikali nambari 1 ya mwaka 2000 kuhusu Sera ya Taifa ya Idadi ya watu kwa Ustawi wa Maendeleo ambayo iliongoza utekelezaji wa mipango ya idadi ya watu hadi mwaka 2010. Sera hii inatambua na kuzingatia athari za idadi ya watu zinazojitokeza kimataifa na kitaifa. Sera hii itachangia kutimia kwa Ruwaza ya Maendeleo ya Mwaka 2030 nchini Kenya kwa kuwa inalenga kupatikana kwa hali ya juu ya maisha kwa watu wa Kenya kwa kusimamia ongezeko la idadi ya watu katika ngazi ambayo inaweza kuhimiliwa na rasilimali zilizopo.

Kubuniwa kwa sera hii kulipitia hatua tofauti tofauti na imejikita katika maoni yaliyokusanywa kutoka kwa wataalam na wadau katika ngazi za mashinani, kimaeneo na kitaifa. Shughuli hii ndefu ilikuwa muhimu kwani ilihusisha viongozi na wadau kote nchini. Ushauri wa wataalam ulichangia kupatikana kwa sera hii ya Idadi ya Watu kwa Ustawi wa Taifa ambayo itatoa mwongozo wa kutekelezwa kwa mipango ya idadi ya watu kuambatana na Ruwaza ya Maendeleo ya Mwaka 2030, Katiba Mpya ya Kenya ya mwaka 2010 na malengo mengine ya kimataifa na kitaifa. Sera hii inagusia sehemu zifuatazo:

- Mfumo wa Idadi ya watu
- Ustawi wa Kiuchumi na Kijamii
- Idadi ya watu na Ustawi wa Mazingira

- Afya ya Uzazi na Haki za Uzazi
- Usawa wa Kijinsia na mamlaka kwa Wanawake
- Magonjwa na Vifo

Inapaswa kuzingatiwa kwamba sera hii inagusia sekta zote na inatoa msingi ambao utakuwa mwongozo kwa mipango ya kitaifa ya idadi ya watu na shughuli zake kwa muda wa miongo miwili ijayo. Utekelezaji wa mipango na miradi kama ilivyopendekezwa katika sera hii, inatoa msukumo wa kushirikishwa kwa sekta za wadau wote.



Mhe. Wycliffe Ambetsa Oparanya, EGH, MP

Waziri katika Wizara ya Mipango, Ustawi wa Kitaifa na Ruwaza ya Maendeleo ya Mwaka 2030

1.0 Nguzo za Sera ya Idadi ya watu kwa Ustawi wa Taifa

Sera hii inalenga kuhakikisha kwamba ongezeko la idadi ya watu halizuii kutimia kwa malengo ya Ruwaza ya Maendeleo ya Mwaka 2030. Inatambulika kwamba idadi ya watu nchini Kenya ambayo iliongezeka kwa asilimia 2.9 katika kipindi cha 1999-2009, ikiwa haitasimamiwa vyema itatatiza juhudi za kuibadilisha Kenya kuwa nchi ya mapato ya kadri. Utekelezaji wa sera hii hivyo basi utaongozwa na nguzo zifuatazo.:

- i. Kuheshimu haki za binadamu na uhuru wao ikiwa ni pamoja na hadhi ya binadamu, usawa na uhuru wa kutobaguliwa kwa misingi ya jinsia, kijamii, kitamaduni na kidini.
- ii. Kutambuliwa kwa familia kama kitengo cha kimsingi katika jamii.
- iii. Kuzingatiwa kwa haki za kimsingi kwa watu wote wakiwemo wale walio katika ndoa kuweza kufanya maamuzi huru juu ya idadi ya watoto wanaohitaji, kupata habari na elimu inayohitajika ili waweze kufanya maamuzi ya busara na kupata kwa urahisi njia za kutekeleza maamuzi yao.
- iv. Kutambuliwa kwa tofauti za kimaeneo kuhusiana na maswala ya idadi ya watu na ustawi wa maendeleo.
- v. Kutambuliwa kwamba jamii zote na watu binafsi wana haki ya kupata nafasi sawa za kujiendeleza.
- vi. Kutambuliwa kwa haja ya kuendeleza usawa wa kijinsia, kuwapa wanawake mamlaka na kumaliza aina zote za dhuluma.
- vii. Kutambuliwa kwa maswala ya kijamii katika sekta mbali mbali na haja muhimu ya mfumo wa kutekeleza maswala hayo katika sekta zote.

2.0 Idadi ya Watu na Hali ya Kijamii na Kiuchumi

Katika kushughulikia changamoto za kiuchumi na kijamii, Kenya ilitekeleza mfumo wa marekebisho ya kiuchumi kama ilivyoratibiwa kwenye Mkakati wa Ufufuzi wa Uchumi na kubuni nafasi za kazi katika kipindi cha mwaka 2003-2007. Hii ilifuatiwa na Mkakati wa Mabadiliko ya kitaifa ya mwaka 2008-2012 ulionuiwa kuongeza kasi ya ustawi wa kiuchumi na kijamii kwa taifa la Kenya. Katika kipindi hiki, juhudi kadhaa za kupunguza umasikini zilianzishwa. Kutokana na hayo, uchumi ulikua kutoka asilimia 0.6 mwaka 2002 hadi asilimia 5.6 mwaka 2010. Ingawaje uchumi wa taifa umekua, mapato ya kibinafsi ya mwananchi yamerudi chini kutokana na ongezeko la idadi ya watu la asilimia 2.9 katika kipindi cha mwaka 1999-2009.

Matokeo ya mwaka 2008/9 ya utafiti wa Watu na Afya (KDHS) pamoja na ripoti ya hesabu ya idadi ya watu na makaazi ya mwaka 2009 yanaonyesha wazi kwamba Kenya imefikia kiwango ambapo idadi ya vifo imepungua na kiwango cha kuzaana kimeongezeka. Kuongezeka kwa kiwango cha uzazi nchini Kenya kumeongeza idadi ya watu wa umri wa ujana. Ili Kenya iweze kupunguza ongezeko la idadi ya watu siku za usoni, kiwango cha uzazi na vifo vya watoto vinahitajika kupungua. Mwaka 2009 idadi ya watu nchini Kenya ilikuwa milioni 38.6. Katika kiwango cha ongezeko la idadi ya watu cha asilimia 2.9 kwa mwaka, idadi ya watu inatarajiwa kuongezeka mara dufu na kufikia milioni 77 ifikiapo mwaka 2030.

Uhamiaji wa watu wa ndani kwa ndani nchini Kenya umesababishwa na tofauti za kiuchumi kati ya maeneo ya kijografia na unatokana na juhudi za kutafuta ajira na makaazi. Uhamiaji huo hasa umekuwa kutoka mashambani hadi mijini japo idadi kubwa ya watu wanaishi mashambani. Ingawaje zamani uhamiaji wa watu kimataifa umechukuliwa kuwa wa kiwango cha chini, kumekuwa na wasiwasi wa uhamiaji wa watu wenye ujuzi hasa kutoka sekta ya afya. Inapasa kuzingatiwa kwamba Kenya inatoa hifadhi kwa idadi kubwa ya wakimbizi kutoka nchi jirani. Kuwepo kwao wakimbizi hao kumbana rasilimali zinazotegemewa na wenyeji.

3.0 Matokeo ya Sera za Idadi ya Watu ya Awali

3.1 Juhudi za Awali

Tangu Uhuru Kenya imebuni sera kadhaa za kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa Idadi ya Watu:

- Mpango wa Kitaifa wa Kupanga Uzazi wa Mwaka 1967
- Mwingozo wa Sera za Idadi ya Watu uliotolewa kupitia Taarifa ya Maongozi Rasmi ya Serikali Nambari 4 ya Mwaka 1984
- Sera ya Kitaifa ya Idadi ya Watu kwa Ustawi wa Maendeleo iliyotolewa kupitia Taarifa ya Maongozi Rasmi ya Serikali Nambari 1 ya Mwaka 2000.

Utekelezaji wa sera hizi ulichangia kupatikana matokeo yafuatayo:

- Kupungua kwa ongezeko la idadi ya watu kutoka asilimia 3.3 mwaka 1984 hadi asilimia 2.9 mwaka 2010
- Kupungua kwa kiwango cha wastani cha watoto kwa kila mama kutoka watoto 7 mwaka 1984 hadi watoto 5 mwaka 2010
- Kupungua kwa vifo vya watoto walio na umri wa chini ya miaka 5 kutoka vifo 115 mwaka 2000 hadi vifo 74 kwa kila watoto 1,000 waliozaliwa mwaka 2010
- Kuongezeka kwa idadi ya kina mama walio kwenye ndoa wanaotumia njia za kupanga uzazi kutoka asilimia 17 mwaka 1984 hadi asilimia 46 mwaka 2010
- Kuongezeka kwa Mpango wa Kitaifa wa Utoaji Chanjo kutoka asilimia 65 mwaka 1998 hadi asilimia 77 mwaka 2009
- Ufahamu juu ya njia za kupanga uzazi ulisalia juu ya asilimia 97
- Kupungua kwa maambukizi ya virusi vya ukimwi kutoka asilimia 6.7 mwaka 2003 hadi asilimia 6.3 mwaka 2009.

3.2 Mambo yaliyochangia ufanisi na pingamizi za utekelezaji sera za awali

Kumekuwa na ufanisi katika utekelezaji wa sera za awali za idadi ya watu ambao umetokana na mambo yafuatayo:

- Kujitolea kwa serikali na misaada kutoka kwa wafadhili
- Kampeni ya hali ya juu
- Kushirikishwa kwa sekta mbali mbali katika shughuli za mipango inayohusu idadi ya watu.

Hata hivyo, utekelezaji wa sera za awali za idadi ya watu umetatizwa na uongozi dhaifu wa kisiasa. Pingamizi nyingine ni pamoja na:

- Viwango vya juu vya umasikini
- Ongezeko la haraka la idadi ya watu
- Kubadilika kwa mwelekeo kutoka afya ya uzazi na mipango inayoshughulikia idadi ya watu baada ya kuzuka kwa janga la UKIMWI
- Kutohusishwa kikamilifu kwa kina mama katika kufanya maamuzi
- Kueleweka vibaya na habari potovu kuhusu njia za kupanga uzazi
- Taarifa za kutofautiana kutoka kwa viongozi wa kisiasa na kidini
- Kupungua kwa misaada ya wafadhili na upungufu wa fedha kutoka kwa serikali
- Uhaba wa ushirikiano baina ya serikali na sekta ya kibinafsi
- Uwezo dhaifu wa taasisi husika kuweza kushirikiana.

3.3 Changamoto zilizopo na zinazochipuka kwa mipango inayoshughulikia idadi ya watu

Kuna changamoto kadhaa zinazojitokeza ambazo zinahitaji kushughulikiwa ili nchi iweze kutimiza malengo yake kama ilivyoratibiwa kwenye Ruwaza ya Maendeleo ya Mwaka 2030 na Malengo ya Ustawi wa Maendeleo ya Milenia hii.

Changamoto ambazo zinaangaziwa kwenye sera hii ya idadi ya watu ni pamoja na:

- Kutofunganishwa kwa matatizo kuhusu idadi ya watu katika mikakati ya maendeleo
- Imani na desturi tofauti tofauti za kitamaduni na kidini zinazohimiza ndoa za mapema na wanaume kuoza wake wengi.
- Idadi kubwa ya Wakenya walio masikini kupita kiasi
- Tofauti kubwa iliyopo ya kimaeneo, kijamii na kiuchumi katika uwezo wa kuzaa, matumizi ya njia za kupanga uzazi na idadi ya vifo.
- Ongezeko la idadi ya watu walio katika umri wa ujana
- Kutohusishwa kikamilifu kwa wanaume katika mipango ya afya ya uzazi na mbinu za kupanga uzazi
- Mabadiliko ya nchi na uwezo wa mazingira kuhimili mabadiliko hayo
- Ukuaji wa miji kwa kasi
- Kutoshirikishwa kikamilifu kwa wanawake katika kufanya maamuzi
- Maradhi ya UKIMWI, Malaria, kifua kikuu na magonjwa mengine yasiyo ya kuambukiza
- Viwango vya chini vya msukumo wa kisiasa katika ngazi za kitaifa na mashinani
- Ongezeko la ukosefu wa usalama na mizozo juu ya rasilimali.

4.0 Maswala kuhusu idadi ya watu na mapendekezo ya hatua za kuchukuliwa

4.1 Mfumo wa Idadi ya watu Nchini Kenya

4.1.1 Ukubwa wa Idadi ya Watu na Ukuaji

Maswala:

- i. Kutokana na ongezeko la idadi ya watu la asilimia 2.9 kila mwaka, idadi ya watu nchini Kenya itafika milioni 77 ifikapo mwaka 2030
- ii. Sehemu kubwa ya wakenya walio na uwezo wa kufanya kazi hawajaajiriwa.

Hatua za kuchukuliwa:

- i. Kuungwa mkono kwa kampeni za kuhamasisha umma juu ya athari za ongezeko la idadi ya watu
- ii. Kuimarisha ufahamu wa kukubali matumizi ya mpango wa uzazi kama mkakati wa kudhibiti ongezeko la idadi ya watu.

4.1.2 Mpangilio wa Idadi ya Watu

(a) Watoto

Maswala:

- i. Kuendeleza mipango na uwekezaji wa hali ya juu unahitajika ili kushughulikia mahitaji ya elimu, afya, chakula, makaazi na ulinzi kwa watoto ambao ni takriban asilimia 55 ya jumla ya idadi ya watu

- ii. Mabadiliko ya kijamii na umasikini yamesababisha ongezeko la idadi ya watoto wanaoishi katika mazingira magumu.

Hatua za kuchukuliwa:

- i. Kuunga mkono utekelezaji wa sera zilizopo na sheria za kulinda haki za watoto
- ii. Kubuni mitaala na vifaa muhimu vya kuanzisha elimu ya idadi ya watoto shuleni na taasisi nyingine za kielimu zinazohudumia watoto walio na umri wa chini ya miaka 18
- iii. Kupigania kutengwa kwa bajeti kwa mahitaji ya kimsingi ya watoto ikiwa ni pamoja na walemavu
- iv. Kuwekwa kwa mfumo wa kisheria unaohakikisha elimu ya msingi ya lazima.

(b) Watu wa Umri Mdogo

Maswala:

- i. Mfumo wa idadi ya watoto walio na umri mdogo huleta msukumo wa ongezeko la idadi ya watoto kwa siku za usoni
- ii. Asilimia 25 ya vijana hawana kazi wavulana wakiwa asilimia 22 huku wasichana wakiwa asilimia 27
- iii. Asilimia tatu ya vijana walio kati ya umri wa miaka 15-24 wanaishi na virusi vya ukimwi huku wanawake wakiwa ndio walioathirika zaidi.

Hatua za kuchukuliwa:

- i. Kampeni za kuunga mkono utekelezaji wa Sera ya kitaifa ya Vijana ikiwa ni pamoja na kupanuliwa na kuimarishwa kwa vituo vya kuwapa ujuzi na mafunzo vijana kuweza kutekeleza mipango maalum ya maendeleo kwa vijana
- ii. Kuimarisha mfumo wa utoaji elimu ya dadi ya Watu na Afya ya uzazi kwa vijana katika sekta zote
- iii. Kupigania kuanzishwa kwa Elimu ya Familia kwa vijana walio ndani na nje ya shule
- iv. Kupigania kuanzishwa kwa mafunzo ya ngazi ya kati na ya juu kubuni ujuzi unaohitajika kwa vijana.

(c) *Watu wa Umri wa Makamo wenye Uwezo wa Kufanya Kazi*

Maswala:

- i. Kutokana na msukumo wa ongezeko la idadi watu, sehemu kubwa ya watoto wanategemea wazazi wachache
- ii. Ongezeko la idadi ya watu wanaotafuta ajira
- iii. Ongezeko la kiwango cha uzazi lithimiza kubuniwa kwa nafasi zaidi za kazi
- iv. Mahitaji ya Mpango wa Uzazi yasiyotimizwa
- v. Idadi kubwa ya watu wanaohitaji Huduma za Afya ya Uzazi.

Hatua za kuchukuliwa:

- i. Kuungwa mkono kwa sera na mipango yenye lengo la kuongeza uwekezaji katika sekta ya elimu na teknolojia, kuanzishwa kwa ubunifu mpya, huduma za afya na miundomsingi kushughulikia sehemu hii ya watu wenye uwezo wa kufanya kazi

- ii. Kuimarisha kampeni ya elimu kuhusu idadi ya watu na kutoa huduma bora za afya ya uzazi ili kutatua mahitaji ya afya ya uzazi kwa wanawake na wanaume
- iii. Kubuni mpango wa kutambua na kuzitua (kuwapa zawadi) familia ndogo.

(d) Wakongwe

Maswala:

- i. Kuporomoka kwa nguzo za kijamii na mifumo inayowasaidia wakongwe
- ii. Kutokuwepo kwa mipango kabambe ya kusaidia wakongwe kutokana na matatizo ya kiuchumi yanayowakabili /yanayokabili familia
- iii. Uwezo mdogo wa kushiriki na kuchangia maendeleo ya taifa.

Hatua za kuchukuliwa:

- i. Kuunga mkono Sera ya taifa kuhusu Ukongwe ikiwa ni pamoja na Kifungu Nambari 47 cha Katiba
- ii. Kupigania upanuzi na usimamizi bora wa hazina ya malipo ya uzeeni na mipango ya bima ya afya
- iii. Kupigania kubuniwa kwa mitandao ya kijamii inayowasaidia wakongwe.

(e) Walemavu

Maswala:

- i. Ukosefu wa miundomsingi ifaayo kwa walemavu kupata kwa urahisi huduma za mpango wa uzazi
- ii. Unyanyapaa na ubaguzi wa kijamii
- iii. Viwango vya juu vya ukosefu wa ajira.

Hatua za kuchukuliwa:

- i. Kuunganisha na kujumuisha maswala yanayoathiri walemavu katika utoaji huduma za afya ya uzazi na mpango wa uzazi katika ngazi zote za jamii
- ii. Kuwekwa kwa takwimu kuhusu mahitaji ya afya ya uzazi na mpango wa uzazi kwa walemavu
- iii. Kupigania kutekelezwa kikamilifu kwa Sheria ya Walemavu ya Mwaka 2003
- iv. Kuanzisha kampeni ya ufahamu kushughulikia unyanyapaa na ubaguzi.

(f) Kusambaa kwa Idadi ya Watu

Maswala:

- i. Takwimu haba kuhusu uhamiaji
- ii. Kuongezeka kwa idadi ya watu masikini katika mitaa ya mabanda mijini
- iii. Uhaba wa huduma za afya ya uzazi kwa watu masikini mijini na sehemu za mashambani na sehemu zisizofikika kutokana na miundombinu mibovu.

Hatua za kuchukuliwa:

- i. Kuunga mkono Juhudi za kukusanya takwimu za uhamiaji
- ii. Kuunga mkono utekelezaji na usambazaji wa huduma na shughuli za kiuchumi chini ya mfumo wa ugatuzi
- iii. Kuunga mkono na kuratibu mipango ya afya ya uzazi inayolenga makundi maalum ikiwa ni pamoja na watu masikini katika sehemu za miji na mashambani pamoja na wale wanaoishi katika sehemu zisizofikika kwa urahisi.

4.2 Maswala kuhusu Mipango ya Idadi ya Watu

4.2.1 Habari, Elimu, Mawasiliano na Upiganiaji

Maswala:

- i. Ukosefu wa ufahamu juu ya uhusiano kati ya familia na matumizi ya rasilimali zilizopo
- ii. Ukosefu wa ufahamu juu ya matumizi ya rasilimali na uhusiano wa ustawi wa mazingira.

Hatua za kuchukuliwa:

- i. Kuimarisha kampeni za ufahamu kwa umma juu ya maswala ya idadi ya watu yanayokumba nchi na kaunti
- ii. Kuboresha ufahamu na msingi wa habari kuhusu maswala ya idadi ya watu
- iii. Kuboresha mfumo wa sera na mazingira ya kukabiliana na maswala ya idadi ya watu
- iv. Kuongeza rasilimali kwa ajili ya mipango inayohusiana na idadi ya watu
- v. Kuimarisha uwezo wa wadau kuweza kupanga, kushirikisha na kutathmini mipango ya idadi ya watu.

4.2.2 Utaoji wa Huduma za Mpango wa Uzazi

Maswala:

- i. Utaoji huduma wa kiwango cha chini
- ii. Uhaba wa njia za kupata vifaa na huduma za kupanga uzazi.
- iii. Ukosefu wa vifaa vya kutosha vya kupanga uzazi kutokana na kutegemea zaidi msaada ya wafadhili.
- iv. Kutojikusisha kikamilifu kwa wanaume katika maswala ya kupanga uzazi.
- v. Hitaji kubwa la kupanga uzazi ambalo halijatimizwa.

Hatua za kuchukuliwa:

- i. Kupanua vituo vya utoaji huduma za mpango wa uzazi vikiwemo vituo vya usambazaji huduma mashinani.
- ii. Kuimarisha ushirikishi wa wanaume katika maswala ya kupanga uzazi
- iii. Kuhakikisha njia mbalimbali za kupanga uzazi zinajumuishwa na vifaa vya kupanga uzazi vinapatikana katika vituo vya utoaji huduma
- iv. Kuimarisha kujumuishwa kwa huduma za mpango wa uzazi, maradhi ya UKIMWI, afya ya uzazi na huduma nyingine za afya.
- v. Kupiganiwa kuongezwa kwa fedha zinazotengewa huduma za idadi ya watu,afya ya uzazi na huduma za mpango wa uzazi.

4.3 Sehemu za Ujumbe Mkuu

4.3.1 Idadi ya watu na ukuaji wa uchumi

Maswala:

- i. Kutojumuishwa kwa maswala ya idadi ya watu katika sehemu zote za mipango ya maendeleo.
- ii. Ugumu wa kupatikana kwa takwimu za idadi ya watu kwa mipango ya maendeleo hasa katika ngazi za chini za maeneo madogo.

Hatua za kuchukuliwa:

- i. Kushirikisha rasilmali ili kuwezesha kupatikana kwa takwimu za idadi ya watu na kutumika kwa takwimu hizo kujumuisha maswala ya idadi ya watu katika sehemu na ngazi zote za mipango ya maendeleo
- ii. Kuimarisha uwezo wa taasisi zinazohusika na ukusanyaji na tathmini ya takwimu kuweza kubuni takwimu zinazoweza kutumiwa kwa ujumuishaji maswala ya idadi ya watu kwenye mipango ya maendeleo katika ngazi zote.

4.3.2 Idadi ya watu na Kupunguza Umaskini

Maswala:

- i. Idadi kubwa ya watu nchini Kenya wanaishi katika hali ya umaskini inayohusishwa na kiwango cha juu cha uzazi na idadi ya juu ya vifo katika sehemu za miji na mashambani
- ii. Kujikokota kwa juhudi za kubuni nafasi za kazi, uchumi wa mali na pengo kubwa kati ya ukuaji wa uchumi na ongezeko la idadi ya watu.

Hatua za kuchukuliwa:

- i. Kuchangia utekelezaji mipango ya kupunguza umasikini kwenye Ruwaza ya Maendeleo ya Mwaka 2030
- ii. Kuboresha utendajikazi wa mipango ya kusitisha ongezeko la kasi la idadi ya watu na kuleta uwiano kati ya idadi ya watu na ukuaji wa uchumi katika ngazi zote.

4.3.3 Idadi ya Watu na Ustawi wa Mazingira

Maswala:

- i. Ujenzi wa makazi ya binadamu katika mazingira dhaifu yakiwemo maeneo ya vyanzo vya maji
- ii. Kutojumuishwa kikamilifu kwa maswala ya idadi ya watu katika mipango ya kutunza mazingira
- iii. Kugawanywa kwa ardhi yenye uwezo wa kuzalisha chakula katika vijishamba vidogo vidogo visivyo na uwezo wa kuhimili uchumi.

Hatua za kuchukuliwa:

- i. Kujumuishwa kwa maswala ya ustawi wa mazingira katika kampeni za ufahamu kuhusu idadi ya watu
- ii. Kuimarishwa kwa matumizi ya takwimu kuhusu idadi ya watu katika mipango ya usimamizi wa mazingira na rasilimali zake
- iii. Kuhimiza ujumuishaji makadirio ya athari za kimazingira katika mipango ya maendeleo na utekelezaji.

4.3.4 Idadi ya Watu, Teknolojia, Utafiti na Maendeleo

Maswala:

- i. Ukosefu wa utafiti unaolenga sera katika ngazi za kitaifa na mashinani, kutambua na kuelewa sehemu zilizo na matatizo ya idadi ya watu kuhusiana na umasikini, mifumo ya matumizi ya rasilimali kupita kiasi na uharibifu wa mazingira
- ii. Rasilimali zisizostahili, kuimarishwa kwa taasisi muhimu za utafiti na ushiriki wa jamii katika sehemu za mashinani
- iii. Ukosefu wa ajenda kamilifu ya Utafiti wa Kitaifa wa Idadi ya Watu
- iv. Uhaba wa utafiti wa kutosha kuweza kushawishi uratibu wa sera na mipango.

Hatua za kuchukuliwa:

- i. Kuimarisha juhudi za kukusanya na kusambaza habari kuhusu idadi ya watu
- ii. Kutoa agenda kamilifu ya kitaifa ya Utafiti wa Idadi ya Watu mara kwa mara
- iii. Kutenga fedha kwa ajili ya utafiti wa idadi ya watu na maendeleo
- iv. Kutoa mafunzo ya mara kwa mara juu ya utafiti, ukusanyaji takwimu na tathmini ya takwimu
- v. Kuimarisha matumizi ya habari kuhusu shughuli za kupanga na uratibu wa mipango na kutoa mafunzo kwa wadau wa matumizi ya habari kuhusu idadi ya watu
- vi. Tathmini mahitaji endelezi ya mafunzo ya juu kuhusu Utafiti wa idadi ya watu

- vii. Kuimarisha uwezo wa kaunti kuweka takwimu na kuzitumia takwimu hizo
- viii. Kuanzisha miradi itakayosaidia kupunguza pengo kati ya utafiti, sera na utekelezaji.

4.3.5 Idadi ya watu na Elimu

Maswala:

- i. Ongezeko la mahitaji ya elimu na mafunzo
- ii. Ongezeko la mahitaji ya walimu wa ziada, wakufunzi na miundomsingi
- iii. Viwango vya chini vya wanafunzi wanaoendelea, wanaoacha na wanaojiunga na masomo kwa ujumla
- iv. Uhaba wa rasilimali unaotatiza juhudi za kupatikana kwa elimu ya msingi kwa wote.

Hatua za kuchukuliwa:

- i. Kupiganiwa kwa mtaala wa elimu uliofanyiwa marekebisho kujumuisha elimu ya familia
- ii. Kuungwa mkono kwa utekelezaji wa sera zinazoimarisha elimu kama vile kurejeshwa shuleni kwa wanafunzi wa kike wanaopata mimba
- iii. Kuboreshwa kwa ufahamu na elimu kwa jamii zinazoendeleza desturi zilizopitwa na wakati kama vile ukeketaji wa wanawake na ndoa za mapema

- iv. Kupigania kuongezwa kwa rasilimali kwa ajili ya elimu katika ngazi zote kwa lengo la kuimarisha elimu iweze kusaidia idadi ya watu
- v. Kulenga kutoa habari kuhusu idadi ya watu kwa taasisi za elimu isiyo rasmi na maeneo yaliyotengwa.

4.3.6 Usawa wa Kijinsia na Kuwapa Wanawake Mamlaka

Maswala:

- i. Kupata elimu
- ii. Kushiriki katika ajira
- iii. Kuzaa na kushiriki katika utunzi wa sera na utoaji maamuzi
- iv. Kuwepo kwa desturi za kitamaduni na kijamii kama vile ndoa za mapema, ukeketaji wa wanawake na miko kuhusu lishe.

Hatua za kuchukuliwa:

- i. Kuimarisha ushiriki wa wanaume na wanawake kufanya maamuzi katika ngazi zote yakiwemo maswala ya afya ya uzazi na mpango wa uzazi
- ii. Kuboresha mazingira ya sera kwa kujumuisha haki za kijinsia na uzazi katika mipango ya idadi ya watu na afya ya uzazi
- iii. Kupigania kuwepo kwa huduma sawa ya malezi kwa waathiriwa wa desturi mbovu zinazodhulumu.

4.3.7 Magonjwa na Vifo

Magonjwa na vifo vya Watoto

Maswala:

- i. Idadi kubwa ya watoto wanaozaliwa na kufariki
- ii. Uhaba wa huduma za chanjo.

Hatua za kuchukuliwa:

- i. Kuunga mkono utekelezaji wa mipango iliyopo ya kulinda maisha ya watoto ikiwa ni pamoja na usimamizi wa magonjwa ya utotoni na juhudi nyingine kama vile kupunguza maambukizi ya virusi vya ukimwi kutoka kwa mama hadi motto na kusambaza vyandarua vya kuinga mbu vilivyotiwa dawa kukabiliana na ugonjwa wa malaria.
- ii. Matokeo yanayotarajiwa ni kwamba maisha ya watoto yanapoimarika, familia ndogo zitakubalika na uwezo wa kuzaa utapungua kwa kiwango kikubwa.

Magonjwa na Vifo vya Wanawake kutokana na uzazi

Maswala:

- i. Idadi kubwa ya wanawake wanaojifungua nyumbani
- ii. Kutoshirikishwa kikamilifu kwa wakunga wakati kina mama wanapojifungua
- iii. Ukosefu wa malezi na vifaa vya kujifungulia kina mama.

Hatua za kuchukuliwa:

Kuimarisha kampeni ya kuongezwa kwa rasilimali za kutoa huduma kamilifu za afya ya kina mama wajawazito kwa kuzingatiwa makundi ambayo hayafikiwi na huduma hizo, kwa kutilia maanani maswala ambayo hayashughulikiwi ikiwa ni pamoja na malezi ya mama kwa kushughulikia matatizo baada ya kujifungua au kuavya mimba.

Maradhi ya UKIMWI, Malaria, Kifua kikuu (TB) na Magonjwa ya Kuambukizwa

Maswala:

- i. Unyanyapaa na kutengwa kwa watu wanaoshi na virusi vya UKIMWI
- ii. Ukosefu wa nafasi ya kupata dawa za kudhibiti makali ya ugonjwa wa UKIMWI
- iii. Malaria bado ni chanzo cha maradhi na vifo vingi nchini Kenya
- iv. Ongezeko la watu wanaouguua ugonjwa wa Kifua kikuu(TB)
- v. Uhaba wa rasilimali.

Hatua za kuchukuliwa:

- i. Kuunga mkono kikamilifu sera na mipango ya Maradhi ya Ukimwi ili kupunguza vifo; kuwezesha kupatikana kwa dawa za kukabiliana na malaria na mipango ya kudhibiti maambukizi ya kifua kikuu na matibabu yake.
- ii. Kujumuishwa kwa jumbe za elimu kuhusu idadi ya watu katika maradhi ya UKIMWI, malaria na Kifua kikuu ili kuweza kutumika kwa rasilimali haba zinazozidi kudidimia.

4.3.8 Afya ya Uzazi na Haki za Uzazi

Maswala:

- i. Imani na desturi za kijamii, kitamaduni na kidini.
- ii. Kiwango cha chini cha wanawake kutoa maamuzi.
- iii. Kutohusishwa kwa wanaume katika maswala ya kupanga uzazi
- iv. Kutokua na uwezo wa kupata watoto
- v. Umaskini
- vi. Mifumo dhaifu ya usimamizi wa afya
- vii. Ufadhili wa kiwango cha chini.

Hatua za kuchukuliwa:

- i. Kuunga mkono utekelezaji wa sera za afya ya uzazi pamoja na sera nyingine zinazounga mkono kupatikana kwa afya na haki ya uzazi kwa wanawake na wanaume
- ii. Kupigania kushirikishwa kwa wanaume na wanawake
- iii. Kuimarisha ufahamu wa haki za jamii kuhusu hali ya kutopata watoto.
- iv. Kupigania kutengwa kwa rasilimali zaidi kuunga mkono mpango wa uzazi
- v. Kushirikisha sekta ya kibinafsi kuunga mkono mipango ya afya ya uzazi.

5.0 Lengo, Madhumuni na Shabaha ya Sera ya Idadi ya watu

Lengo, nia na shabaha ya sera hii inalenga taswira nzima ya Ruwaza ya Maendeleo ya Mwaka 2030.

5.1 Lengo la Sera

Lengo ni kupatikana kwa hali ya juu ya maisha ya watu wa Kenya kwa kusimamia ongezeko la idadi ya watu ambayo rasilimali zilizopo zinaweza kuhimili.

5.2 Madhumuni ya Sera

- i. Kupunguza kiwango cha ongezeko la idadi ya watu kuweza kuwiana na ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii kuambatana na Ruwaza ya Maendeleo ya Mwaka 2030
- ii. Kupunguza idadi ya vifo vya watoto wakati wa uzazi, vifo vya watoto wa umri wa chini ya miaka 5 na vifo miongoni mwa wanawake wakati wa kubeba mimba na wakati huo huo kuwasaidia watu binafsi na wale walio katika ndoa wanaohitaji watoto lakini hawawezi
- iii. Kutoa habari na elimu juu ya maswala ya idadi ya watu kwa umma na hasa vijana kuhimiza fikra na ushawishi wa kuwa na familia ndogo
- iv. Kutoa huduma za afya ya uzazi za gharama ya chini kwa wote ikiwa ni pamoja na mpango wa uzazi
- v. Kuchangia mpango wa uzazi na utekelezaji wa mipango ya ustawi wa kiuchumi na kijamii
- vi. Kushirikisha rasilimali kupitia bajeti ya serikali, ushirikiano wa wafadhili wa kimataifa na ushirikiano wa sekta ya umma na ya kibinafsi.

5.3 Shabaha za mwaka 2030

Shabaha zilizotajwa zitaongoza utekelezaji wa mipango ya idadi ya watu kwa miaka ijayo. Makadirio haya yatajumuisha kipindi cha mwaka 2010 hadi 2030 na yatafanyiwa marekebisho ya mara kwa mara kukizuka mahitaji.

Shabaha hizi ni:

- i. Kupunguza ongezeko la idadi ya watu kutoka asilmia 2.5 mwaka wa 2009 hadi asilmia 1.5 ifikiapo mwaka 2030.
- ii. Kupunguza vifo miongoni mwa watoto walio na umri wa chini ya mwaka mmoja kutoka 52 mwaka 2009 hadi 25 kati ya watoto 1,000 wanaozaliwa hai kufikia mwaka 2030
- iii. Kupunguza kiwango cha vifo vya watoto walio na umri wa chini ya miaka 5 kutoka 74 mwaka 2009 hadi 48 kati ya watoto 100,000 wanaozaliwa hao kufikia mwaka 2030
- iv. Kupunguza idadi ya vifo miongoni mwa wanawake wakati wa kubeba mimba au wanapojifungua kutoka 488 mwaka 2009 hadi 200 kwa kila wanawake 100,000 wanaojifungua kufikia mwaka 2030
- v. Kupunguza kiwango cha wastani cha vifo kote nchini Kenya kutoka 13 mwaka 2010 hadi 8 kwa kila watu 1,000 kufikia mwaka 2030
- vi. Kuboresha muda wa miaka anayotarajiwa mtu kuishi kutoka kuzaliwa kwa jinsia zote kutoka 57 mwaka 2009 hadi miaka 64 kufikia mwaka 2030

- vii. Kupunguza kiwango cha wastani cha watoto wanaozaliwa na kila mwanamke kutoka 5 hadi watoto 3 kufikia mwaka 2030
- viii. Kupunguza asilimia ya wasichana wanaopata mimba mapema kutoka asilimia 15 mwaka 2009 hadi asilimia 7 kufikia mwaka 2030
- ix. Kupunguza idadi ya vijana wanaopata watoto kutoka asilimia 18 mwaka 2009 hadi asilimia 8 ifikapo mwaka 2030.

6.0 Utekelezaji, Uangalizi na Tathmini

Sera hii itatekelezwa katika misingi ya Ruwaza ya Maendeleo ya Mwaka 2030 na Katiba mpya ya mwaka 2010. Hata hivyo utekelezaji wake utahusisha Serikali, Mashirika ya Kijamii, Mashirika yasiyo ya serikali, Sekta ya Kibinafsi na Jamii kwa jumla. Baraza la Kitaifa la Idadi ya Watu na Maendeleo litakuwa mshauri mkuu katika utekelezaji wa sera hii. Sera hii itaimarisha uhusiano miongoni mwa wadau kuwezesha matumizi kamilifu ya rasilimali na kupunguza kutekelezwa kwa juhudi kama hizo na wadau wengine. Pia itahakikisha kwamba juhudi za wadau zinawianishwa kuhakikisha malengo ya idadi ya watu yanatimia. Ili kuweza kwenda sambamba na utekelezaji wa Ruwaza ya Maendeleo ya Mwaka 2030, sera hii itatekelezwa katika awamu 4, kila awamu ikichukua muda wa miaka mitano (2011-2015, 2016-2020, 2011-2025 na 2026-2030)

Mfumo wa uangalizi ni muhimu kwa utekelezaji wa sera hii. Mfumo huo utaboresha utoaji maamuzi yanayowahusu wadau katika ngazi zote. Takwimu na habari kutoka mfumo wa uangalizi zinapasa kuhimiza mawasiliano na utangamano kati ya wadau tofauti tofauti wanaohusika katika mahitaji ya kaunti na kitaifa. Mfumo huo unapaswa kuingiliana na mfumo wa kitaifa wa uangalizi na tathmini. Kwa jinsi hii Baraza la kitaifa la Idadi ya Watu na Maendeleo litafanya kazi kwa karibu na wizara husika, mashirika ya serikali, sekta ya kibinafsi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kubuni mwelekeo wa mfumo wa uangalizi na mipango kuhakikisha kuna uangalizi na tathmini ya utekelezaji wa sera hii katika ngazi zote.

Shirika la Kitaifa la Ushirikishi wa Idadi ya Watu na Maendeleo

S.L.P. 48994 - GPO, Nairobi 00100, Kenya

Simu: 254 20 271 1600/01

Kipepesi: 254 20 271 6508

Baruapepe: info@ncpd-ke.org

www.ncpd-ke.org

NCPD ni shirika la Serikali linalobuni na kuimarisha sera za idadi ya watu na kushirikisha shughuli zinahusiana kwa ustawi wa maendeleo nchini Kenya.